BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI
NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)

# JARIDA LA NOVEMBA, 2024

TOLEO: 0003 TAREHE 30 NOVEMBA, 2024

## NACTVET YATAHADHARISHA WANANCHI VYUO 'FEKI'




Baraza la Taifa la Elimu la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limetoa rai kwa wananchi kuchukua tahadhari wanapowatafutia watoto wao nafasi za masomo kwenye vyuo vinavyojitangaza kutoa mafunzo.

Rai hiyo imetolewa Novemba 24, 2024 na Meneja Uthibiti Ubora wa NACTVET, Mhandisi Enock Kayani, akiwa kwenye ukaguzi wa Chuo cha KEWOVAC kilichopo Mbagala, jijini Dar es Salaam, kinachodaiwa kujihusisha na utoaji mafunzo ya uuguzi na ukunga, bila ushahidi wa usajili wa chuo hicho kwenye rejesta ya vyuo vinavyotambuliwa na NACTVET.

Chuo cha KEWOVAC kimegundulika kutosajiliwa na kukosa miundombinu yenye kukidhi sifa za kutoa mafunzo ya uuguzi na ukunga na kuwa na mazingira hatarishi kwa wanafunzi wake.
Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mhe. Sixtus Mapunda, mnamo tarehe 21 Novemba, 2024, alitoa agizo chuo cha KEWOVAC kusitisha mafunzo baada ya kugundulika kuwa kinatoa mafunzo bila kusajiliwa na kukosa mtaala wa mafunzo kinachodaiwa kuyatoa.

Mha. Kayani na timu yake ametanabaisha kwa kusema, "Mazingira ya chuo hayaridhishi na kwa kweli, Mhe. DC alifanya vyema kukifungia chuo hiki... Sisi kama Taasisi

inayojihusisha na ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi tunaona kabisa kuna tatizo."

Amesema timu ya NACTVET imekagua maeneo mbalimbali ya chuo, ikiwemo madarasa na mabweni, na kujionea hali halisi ya kujifunza na ujifunzaji isivyoridhisha, licha ya wanafunzi hao kufundishwa programu ambayo haipo baada ya kuondolewa kwenye mpango wa ufundishaji miaka mitatu iliyopita.



Meneja huyo wa uthibiti ubora amewasihi wazazi kujiridhisha kwanza na usajili wa vyuo vinavyojitangaza kabla ya kuwapeleka watoto wao kuchukua mafunzo yoyote ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.



Aidha, amewataka wazazi wenye watoto chuoni hapo kuwaondoa mara moja.

Wakati huo huo, Afisa Mtendaji wa Kata ya Nzasa, Bi Adela Kalolela, amesema kuwa awali wananchi waliaminishwa kuwa chuo hicho kimesajiliwa na kinaendesha mafunzo halali kulingana na taratibu, kabla ya Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mhe. Sixtus Mapunda kufika chuoni hapo na kutangaza kukifungia mnamo tarehe 21 Novemba, 2024.



Agizo la Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mhe. Sixtus Mapunda, Novemba 21, 2024 lilikuwa la kukifungia chuo cha KEWOVAC hadi kitakapofanya maboresho ya miundombinu na kuweka mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia.



Hata hivyo, Uongozi wa Chuo haukuweza kupatikana kujibu tuhuma hizo. Aidha, wanafunzi waliokutwa kwenye mabweni hawakuweza kutoa ushirikiano kwa watumishi wa NACTVET walipotaka kuzungumza nao.

# MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR YATEMBELEA NACTVET



Viongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar (VTA), walitembelea Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) tarehe 19 Novemba, 2024, kwa lengo la kujifunza kuhusu masuala mbalimbali ya usimamizi na utoaji wa mafunzo ya amali.

Ujumbe huo, ulioongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa VTA, Dkt. Bakari Silima, ulikutana na kufanya mazungumzo na Menejimenti ya NACTVET katika ofisi za Kanda ya Mashariki, jijini Dar es Salaam.



Dkt. Silima alieleza kuwa VTA inatambua umuhimu wa kushirikiana kwa karibu na NACTVET ili kujifunza na kupata uzoefu zaidi katika masuala ya urekebu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali). Amesisitiza kuwa lengo ni kuzalisha wahitimu mahiri watakaoweza kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi kitaifa na kimataifa.

Mkurugenzi huyo, aliainisha maeneo ya kipaumbele ambayo VTA inahitaji kujifunza kutoka NACTVET, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa Amali, uanzishwaji wa programu za Stashahada katika mafunzo ya amali, pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Awali, Katibu Mtendaji wa NACTVET, Dkt. Adolf Rutayuga, alitoa wasilisho kwa ujumbe wa VTA, akieleza shughuli mbalimbali zinazofanywa na Baraza na kuzungumzia urekebu unaofanywa na NACTVET kwenye vyuo vya Kati upande wa Zanzibar.

Dkt. Rutayuga aliuhakikishia ugeni huo kuwa NACTVET iko tayari kushirikiana kwa karibu na VTA na kutoa ushauri katika masuala mbalimbali yanayohusu utoaji wa mafunzo ya

amali kwa kuzingatia ubora wa mafunzo hayo kwa pande zote mbili.











Mazungumzo hayo, yaligusia kuingiwa makubaliano ya awali kuhusu kuanzisha ushirikiano rasmi kati ya NACTVET na VTA, ambapo maeneo yote ya kipaumbele yataainishwa na hatimaye, Makubalino ya Ushirikiano (MoU) kusainiwa.

# WAMILIKI, WAJUMBE WA BODI NA WAKUU WA VYUO VYA UFUNDI ZANZIBAR WAJENGEWA UWEZO



Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limevitaka vyuo vya Ufundi Zanzibar kuhakikisha vinazingatia utawala bora na uadilifu katika uendeshaji wa vyuo vyao na utoaji mafunzo yenye ubora ili kuzalisha wahitimu wenye tija.



Rai hiyo ilitolewa tarehe 7 Novemba, 2024 huko Unguja, Zanzibar, na Meneja wa Kanda ya Mashariki wa NACTVET, Dkt. Obeid Mahenya, kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa NACTVET, Dkt. Adolf Rutayuga, wakati wa ufunguzi wa warsha ya kuwajengea uwezo wamiliki, wajumbe wa bodi na wakuu wa vyuo vya ufundi Zanzibar kuhusu masuala ya uongozi, uadilifu na maadili.

Dkt. Mahenya alisema tathmini iliyofanywa na NACTVET imebaini upungufu wa maarifa katika nyanja za utawala, uongozi na usimamizi wa vyuo. Amesema hali hiyo imekuwa ikiathiri utoaji mafunzo bora ya ufundi, yaliyo muhimu katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa nchi.

Alibainisha kuwa Baraza hilo linaendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini mara kwa mara kwenye vyuo linavyovisimamia kote nchini, ili kuhakikisha wanafunzi wanaojiunga kwenye vyuo wanapata elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora stahiki.

Dkt. Mahenya alisisitiza kuwa NACTVET itaendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi zote za mafunzo ya ufundi Zanzibar ili kuhakikisha programu hizo zinakidhi mahitaji ya uchumi wa taifa, na hivyo kuzalisha nguvu kazi inayoweza kukidhi mahitaji ya kazi katika dunia inayobadilika kwa kasi.

Wakati huo huo, Afisa Mipango kutoka Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ndg. Ussi Jecha Haji, aliipongeza NACTVET kwa

kuandaa warsha hiyo inayolenga kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika uendeshaji wa vyuo. Amewasihi wasimamizi wa vyuo kutoa ushirikiano kwa Wizara na Wadhibiti Ubora, na kuwa tayari kupokea ushauri, na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na NACTVET ili kuboresha utoaji wa mafunzo.



Naye mmoja wa washiriki wa warsha hiyo, ambaye ni Mkuu wa Chuo cha 'Glorious Polytechnic College', Dkt. Idrisa Muslim Hija, alibainisha kuwa mafunzo hayo yatasaidia kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa vyuo.



Kwa upande wake Meneja wa NACTVET Zanzibar, Bi. Elitha Mbedule, alisisitiza kuwa viongozi wa vyuo wanao mchango mkubwa katika kufanikisha utoaji mafunzo na kuelezea matumaini yake kwamba warsha hiyo itawaongezea uwezo na maarifa katika utendaji kazi.

# MAANDALIZI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA ESPJ II: WADAU WAJADILI MASUALA YA JAMII NA MAZINGIRA



Wadau mbalimbali wa elimu wamekutana tarehe 21 Novemba, 2024 kujadili na kuweka mikakati ya kushughulikia masuala ya jamii na mazingira ikiwa ni sehemu muhimu ya maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi Awamu ya Pili (Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ II).



Akizungumza wakati wa warsha hiyo ya wadau iliyofanyika katika ofisi za NACTVET Kanda ya Mashariki jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Mradi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Erick Mgaya, amesema kuwa ufanisi wa utekelezaji wa mradi huo unategemea sana ushiriki mpana wa jamii na umakini katika masuala ya mazingira. Amesisitiza kuwa, ili kufanikisha malengo ya mradi, ni muhimu kuwa na mkakati madhubuti utakaowezesha kuzingatia masuala hayo kwa ufanisi.

Mradi wa ESPJ II unalenga kuimarisha mifumo ya kusimamia ujuzi pamoja na kuboresha mafunzo ili yaendane na mahitaji ya soko la ajira na hatimaye kuzalisha wahitimu mahiri ambao watakuwa na uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa.



Mradi huo, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, unatarajia kunufaisha wananchi milioni 1.5

nchini kwa kuwapa ujuzi katika sekta za Kilimo, Afya, Ujenzi, Uchukuzi, Nishati, Mawasiliano, Madini, Mifugo na Uvuvi, Viwanda pamoja na Utalii na Ukarimu. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka mitano kuanzia 2025 hadi 2030.



Miongoni mwa washiriki wa warsha hiyo ni Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Shirika lisilo la Kiserikali la Uwezo Tanzania, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Shirika la World Vision, Taasisi ya DonBosco, Shirika la Kujitolea la Kimataifa la VSO pamoja wataalam kutoka Benki ya Dunia.

# NACTVET YASHIRIKI KWA MARA YA KWANZA MASHINDANO YA SHIMMUTA 2024




Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limeshiriki kwa mara ya kwanza Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi (SHIMMUTA), yaliyofanyika mkoani Tanga kuanzia tarehe 10 hadi 24 Novemba, 2024.

Michuano ya SHIMMUTA, inayofanyika kila mwaka, iliwaleta pamoja wafanyakazi kutoka sekta mbalimbali ambao walishiriki katika michezo ya aina tofauti ikiwemo mpira wa miguu, netiboli, riadha, bao, vishale, mpira wa wavu, vishale, drafti na michezo mingine mingi. Mashindano ya mwaka huu yalivutia idadi kubwa ya washiriki kutoka Taasisi za umma na binafsi 92.

NACTVET ilishiriki katika michezo ya netiboli, mpira wa wavu, riadha, kuvuta kamba, bao, drafti na 'pooltable' ambapo katika michezo hiyo, NACTVET ilifanikiwa kupata ushindi katika hatua za awali za makundi katika michezo ya karata, pooltable na bao ingawa haikufanikiwa kuingia katika hatua ya 16 bora.

Mashindano ya SHIMMUTA yalifunguliwa rasmi tarehe 18 Novemba, 2024, na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe Dkt. Doto Biteko, ambaye aliwaelekeza viongozi wa Taasisi za Umma kuhakikisha wanatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kushiriki katika Mashindano ya SHIMMUTA. Alisisitiza kuwa ushiriki katika michezo hiyo utachangia kuongeza ufanisi mahali pa kazi pamoja na kuboresha afya za wafanyakazi.

Pamoja na hilo, Mhe. Dkt. Biteko aliiagiza Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni, kukamilisha Sera ya Michezo Mahali Pa kazi,

ili kuwabana waajiri wasiotambua umuhimu wa sekta hiyo kwa watumishi na kuacha kutumia sababu ya ufinyu wa bajeti kama kikwazo cha wafanyakazi kutoshiriki katika michezo hiyo wakati viongozi wa taasisi hizo wamekuwa wakishiriki ziara zikiwemo za mafunzo na semina nje ya maeneo yao ya kazi wakigharamiwa na taasis zao.







“Kuna waajiri na menejimenti ambazo, licha ya Serikali kuweka utaratibu wa michezo inayohusisha asasi za umma na binafsi, wanashindwa kuwawezesha watumishi wao kushiriki, kwa sababu zisizokuwa na uzito, ikiwemo ufinyu wa bajeti,” alisema.



Mshindano ya SHIMMUTA yalihitimishwa rasmi tarehe 24 Novemba, 2024 na Naibu Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Stanslaus Nyongo, kwa kugawa zawadi kwa washindi ikiwemo Vikombe na Medali na kuwahimiza Wakuu wa Taasisi za Umma nchini kuhakikisha wanawaruhusu wafanyakazi wao kushiriki mashindano ya SHIMMUTA ili kuimarisha afya na kuleta ufanisi mahala pa kazi.





Naye, Katibu Mtendaji wa NACTVET, Dkt. Adolf Rutayuga, ambaye alishiriki halfa hiyo amesema, Baraza linatambua umuhimu wa mashindano hayo na litaendelea kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa kuwaruhusu wafanyakazi wake kushiriki mashindano hayo na amewataka wawakilishi wa mwaka huu kutoka NACTVET kuanza maandalizi mapema kwa mashindano ya SHIMMUTA mwakani.

# IFAHAMU NACTVET

**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ni Taasisi iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, Sura 129 na Marekebisho yake ya mwaka 2021 na kupewa jukumu la kusajili, kutoa ithibati, kuthibiti ubora na kuratibu utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini.**

+255 26 232 3121
+255 733 777 751
+255 736 310 311

P. O. Box 17007,
NSSF Building - 3rd Floor,
Mwangosi Road,
41110 Kilimani, Dodoma.

info@nacte.go.tz

www.nactvet.go.tz

nactvet

**"NACTVET - UJUZI, UBORA, UMAHIRI"**